# LIKIZO YA KULIPIWA YA MINNESOTA

**Itaanza kufanya kazi tarehe** 1 Januari, 2026

**Likizo ya Kulipiwa ya Minnesota inatoa malipo na ulinzi wa kazi wakati unahitaji mapumziko ili kuenda kujitunza au kuitunza familia yako.**

## Je, ninaweza kutumia Likizo ya Kulipiwa kufanya nini?

Likizo ya Matibabu:

- Kutunza hali mbaya ya afya yako, ikiwa i pamoja na utunzaji unaohusiana na ujauzito, kujifungua na kupona.

Likizo ya Familia:

- **Likizo ya Mapatano** – kutunza na kupatana na mtoto mgeni kwa njia ya kuzaliwa, kuasili au makao ya kulea.
- **Likizo ya Utunzaji** – kumtunza mwanafamilia aliye na hali mbaya ya afya
- **Likizo ya Familia ya Jeshi** – kumsaidia mwanafamilia aliyeitwa kutoa huduma
- **Likizo ya Usalama** – kukabiliana na matatizo yanayohusiana na dhuluma za nyumbani, ubakaji, au kujichunguza au kumchunguza mwanafamilia

Kwa jumla, lazima hali zidumu zaidi ya siku saba na ziidhinishwe na mtoa huduma wa afya au mtaalamu mwingine.

## Je, ninafidiwa na Likizo ya Kulipiwa?

Wafanyakazi wengi katika jimbo la Minnesota wanafidiwa na Likizo ya Kulipiwa. Unafidiwa bila kujali ukubwa wa mwajiri wako, au saa au siku unazofanya kazi. Wakandarasi wa binafsi na watu waliojiajiri hawafidiwi moja kwa moja lakini wanaweza kujiunga. Huenda ukastahiki malipo ikiwa umelipwa kiasi cha chini kwa ajili ya kazi katika jimbo la Minnesota mwaka mmoja uliopita ($3,900 za kuanza kwa Likizo ya Kulipiwa mwaka wa 2026).

## Je, ninaweza kuenda likizo kwa muda gani?

Huenda ukastahiki kuenda hadi wiki 12 za likizo ya familia au matibabu kwa mwaka wa mafao. Ukihitaji likizo ya familia na matibabu katika mwaka uo huo wa mafao, huenda ukastahiki hadi wiki 20 kwa jumla.

## Je, nitalipwa kiasi gani?

Unapotumia Likizo ya Kulipwa, jimbo linakutumia malipo. Likizo ya Kulipiwa italipa hadi 90% ya mishahara yako, kulingana na kiwango chako cha mapato, kwa kiasi cha juu zaidi cha kila wiki kilichobainishwa kwa mshahara wa wastani wa jimbo wa kila wiki. Kiasi hiki hubadilika kila mwaka na ni $1,423 kwa mwanzo wa Likizo ya Kulipiwa mwaka wa 2026.

## Je, ni nani anayelipia Likizo ya Kulipiwa?

Likizo ya Kulipiwa inafadhiliwa na ada za bima ambazo waajiriwa na waajiri hulipa. Ada ya bima ya mwanzo ni 0.88% ya mishahara inayofidiwa. Mwajiri wako anaweza kudondoa hadi 0.44% ya mishahara yako kufadhili sehemu ya ada ya bima.

## Je, ulinzi wa ajira yangu ni gani?

- **Ulinzi wa kazi**: Kwa jumla, lazima urejeshwe kwenye kazi yako au nafasi sawa unaporudi kutoka kwenye likizo. Ulinzi wa kazi unaanza kufanya kazi siku 90 baada ya tarehe yako ya kuajiriwa.
- **Kuendelea kwa bima ya afya**: Kwa jumla, lazima waajiri waendelee kufadhili sehemu yao ya ada za bima ya afya ukiwa kwenye likizo.
- **Hakuna ulipizaji kisasi wala uvurugaji**: Lazima waajiri waepuke kuvuruga au kulipiza kisasi dhidi yako ukituma ombi la au ukitumia Likizo ya Kulipiwa. Waajiri hawawezi kuchukua malipo yako ya Likizo ya Kulipiwa.

Kwa maswali yanayohusiana na Likizo ya Kulipiwa, tafadhali wasiliana na Minnesota Paid Leave (Likizo Ya Kulipiwa Ya Minnesota) kwa nambari 651-556-7777 au tembelea tovuti yetu.

Ikiwa unadhani kwamba mwajiri wako anakiuka ulinzi wa ajira, wasiliana na Kitengo cha Viwango vya Kazi kupitia Idara ya Kazi na Viwanda ya Minnesota.

**PATA MAELEZO ZAIDI:** paidleave.mn.gov

Taarifa hizi zinaweza kutolewa katika miundo mbadala kwa watu walio na ulemavu au watu wanaohitaji usaidizi wa lugha kwa kupigia simu Kituo cha Mawasiliano cha Likizo ya Kulipiwa kwa nambari 651-556-7777 au 844-556-0444 (simu bila malipo).

MINNESOTA PAID LEAVE

Minnesota Paid Leave | 180 E 5th St Suite 1200 | Saint Paul, MN 55101

11/2025